

SABABU NYINGINE YA YESU KUBAKI SIKU 40

AKIWATOKEA WANAFUNZI WAKE NI ILI AONDOE

HALI YA MATABAKA WALIYOKUWA NAO.

MAANDIKO: YOH. 20:11-18, MDO. 1: 12-14, MARK.16: 9 -11

- Kitendo cha Yesu cha kuwaunganisha Wanawake na Wanaume ili wasali pamoja, chumba kimoja lilikuwa ni jambo kubwa ambalo lilikuwa halijawahi kutokea katika Israeli!!! Muda wote aliotembea nao alishuhudia ubaguzi wa hali ya juu kwa wote waliokuja kwa Bwana Yesu ili awahudumie. **Math. 14: 14 -21 (Mark. 6: 30- 44, Mark. 8: 1 - 10 n.k.**
- Yesu alijua (alifahamu) fika kwamba ili kazi ya Injili ipate kusonga mbele, wanaume peke yao hawataweza ni wanawake ndiyo waliokuwa wakimhudumia hata yeye kwa mali zao na kuwaacha kando hawa, alifahamu kwamba injili itakwama tu. **Luk. 8: 1 - 3, Yoh. 12: 1 - 8.**

Note: Eneo la Watumishi wa Mungu kuhudumiwa na wanawake katika Biblia na huduma zao kuimarika ni nyingi mno.

Mfano: 2Wafal. 4: 8 - 17, 1Wafal. 17: 10 -16.

- **Unajua:** Yesu aliita wanafunzi wake waliokuwa na tabia tofauti tofauti kabisa na uelewa wa mambo tofauti tofauti kabisa; wengine walikuwa wavuvi tu wasio na elimu yoyote; wengine wasomi na wanasheria, wengine wasomi wa sheria za kodi n.k. wote hawa bila kuwaunganisha na kuondoa tofauti zao ili wafanye kazi ya injili kama timu moja ili kuleta ushindi wa Injili duniani, nini kingetokea? **Mark. 3:13** au kama Yesu asingebaki ili kutatua tatizo la Mtume Petro (Mzee aliye na umri mkubwa kuliko wote) na Yohana Kijana mdogo kuliko wote lakini ndiye aliyekuwa anapendwa sana na Yesu na kuegema kwenye kifua chake wakati wote!!! **Yoh. 21: 20 - 23, Yoh. 13: 21 - 26.**

Note: **John. 20-23: To be like Peter is Honourable. To be like John (beloved disciple is desirable; but to be in the Lord's will is profitable;)** yaani kuwa kama Petro ni **heshima**; kuwa kama Yohana mwanafunzi aliyependwa sana na Yesu **inapendeza**; lakini kuwa katika mapenzi makamilifu ya Mungu **kunafaa** sana (kuna faida sana)

- Alihakikisha **mashindano** yaliyokuwa katikati yao ya nani **mkubwa** kuliko mwingine yameondoka; nani **bora** kuliko mwingine ikaondoka, na badala yake akapanda roho ya kila mmoja kumwona mwingine kuwa bora kuliko yeye. **Filip. 2: 2 – 4; (Math. 20:20-28)**
- Sote tunafahamu kwamba mgawanyiko wa Taifa la Israel ulisabishwa na Mfalme **Rehoboamu** aliyethamini vijana zaidi katika utawala wake na kupuuza wazee!!! **1Wafal.12: 1 – 24.**
- Mfalme Rehoboamu alikosa **OIKOS** (neno la kuwaunganisha tu -) wakagawanyika!! hata alipojaribu kutumia jeshi na nguvu kuwatawala, alikwama.

NB: Yesu alifahamu nafasi ya kila kiungo na umuhimu wake ndiyo maana alifanya kazi kubwa sana ya kuwaunganisha ili wawe kitu kimoja na kuweka pembeni kabisa tofauti zao, kisomo na wale wasio na kisomo, tofauti zao za kiume au kike na ndiyo sababu siku ya Pentekoste wote wakajazwa na Roho Mtakatifu. Mdo. 2:1 – 4.

- Hata Mitume walipotaka kurudiwa tena na roho hii ya kibaguzi baadae, Mungu alimwinua Yusufu (Baranaba) ili kuwasaidia na wakaelewa. **Mdo. 9:26-31 (Mdo. 4: 36 – 37).**

- Hata Mtume Paulo alipojisahau na kutaka kujiona bora na kutomthamini Marko katika kazi ya Injili, bado Barnaba alimsaidia kwa vitendo. **Mdo. 13: 13, 15: 36 – 41.**
- Bila kuwepo kwa Barnaba, hasara gani leo Kanisa lingekuwa nayo kwa kuzikosa nyaraka zote muhimu alizoziandika Mtume Paulo!!!
- **Warumi, 1Kor, 2Kor, Galatia, Efeso, Filipi, Kolosai, 1Thes. 2Thes. , 1Timoth, 2Timoth, Tito, Filemon, Waebrania,!!!!** lakini pia Kanisa lingekosa kitabu cha Injili ya Marko.!!!!

NB: MWL. NYERERE ALIFAILU SNAA KATIKA JAMBO HILI LA KUTUUNGANISHA WATANZANIA.

Mwisho:

Bwana atupe ufahamu huu wa kuthaminiana na kumwona mwingine kuwa bora kuliko mimi ili kazi ya Mungu ipate kusonga mbele daima. **1Kor. 12: 12 – 27. Amina.**

Askofu Dr. L. Mwizarubi
April 2021